*SWAHILI FORUM 27 (2020): 32-56*

# SITIARI KATIKA *KICHOMI* – UCHAMBUZI WA MOJAWAPO YA MBINU ZA KIFASIHI YA EUPHRASE KEZILAHABI[*]

**KULIKOYELA K. KAHIGI**

Makala hii inachambua sitiari katika Kichomi, diwani ya kwanza ya marehemu Euphrase Kezilahabi. Mashairi yaliyochunguzwa yanahusika na dhamira tatu za kijumla: maana ya maisha, udhalimu wa kikoloni, na hali ya sasa ya Afrika. Mashairi yanayochambuliwa ni: "Nimechoka", "Mwamba Ziwani", "Fungueni Mlango", na "Kisu Mkononi" (dhamira ya "maana ya maisha"); "Hadithi ya Mzee" (dhamira ya "udhalimu wa kikoloni"); "Afrika na Watu Wake", "Kumbe", na "Namagondo" (hali ya sasa ya Afrika). Mashairi haya yako kwenye muundo usiofuata urari wa vina na mizani. Lengo la makala hii si kufanya uchambuzi wa kina bali ni kuonyesha kuwa sitiari ni mbinu ya msingi ya mshairi katika kuwasilisha maana na mtazamo wake katika dhamira kadhaa. Nimeteua mashairi hayo tu ili kudhihirisha mbinu ya kisitiari katika dhamira zilizotajwa. Uchambuzi wa sitiari umezingatia mkabala wa kisemantiki unaotambua vipengele vitatu katika muundo wa sitiari: *kifananishi*, *kitajwa* na *kiungo* (taz. Richards 1936; Leech 1969). Hitimisho muhimu ni kwamba sitiari ni mbinu inayoyawezesha mashairi hayo kuchanuza mawazo na hisia kwa uwazi na athari nzito.

## Utangulizi

Marehemu Euphrase Kezilahabi ni miongoni mwa washairi maarufu wa Kiswahili ambao wamepata kutunga mashairi bora ya kimamboleo. *Kichomi*, diwani ya kwanza ya Kezilahabi, ilitoka mwaka 1974, na kutangaza ushairi usiofuata kanuni za kimapokeo. Akitangaza kanuni ya kisanaa aliyoizingatia, Kezilahabi anatamka: "Jambo ninalojali sana katika ushairi ni utumiaji wa picha au taswira"[1] (Dibaji, Kezilahabi 1974: xiv). Picha au taswira ni dhana pana. Katika makala hii, nimechagua kushughulikia kipengele kimoja tu cha taswira: *sitiari*.

Sitiari ni kipengele kilicho na uzito sana kifani katika ushairi na fasihi kwa jumla (taz. Richards 1936; Ullmann 1964; Nowottny 2000; Semino & Steen 2008) na kwa hiyo kinastahili

[*] Makala hii inatokana na utafiti wa zamani sana (Kahigi 1976, 1977). Hata hivyo, nimeongeza marejeleo machache ya miaka ya hivi karibuni. – *Mwandishi*. ***** Makala hii imeandikwa kama makala ya kumbukizi. Imetokana na kazi maalumu mbili za mwandishi ambazo hazijachapishwa (taz. hapo juu) na ambazo tumepata fursa ya kuzisoma. Imewasilishwa kama mchango maalumu kwa ajili ya heshima ya Marehemu Profesa Euphrase Kezilahabi ikionyesha wazi kwamba kazi za Marehemu zilianza kuchambuliwa mapema na wanafunzi wa fasihi ya Kiswahili wa wakati ule ambao waliungana naye kama wahadhiri wenzake Chuo Kikuu muda mfupi baadaye na pia kuwa washairi wenzake katika mkondo mpya wa wakati huo usiofuata urari wa vina na mizani. Tunamshukuru sana mwandishi kwa kuchangia makala hiyo katika jarida letu la *Swahili Forum*. – *Wahariri*.

[1] Kuifanya taswira kuwa 'kanuni ya msingi ya kiujumi' katika ushairi si jambo geni. Washairi na wahakiki wengi wameshatamka hivyo; kwa mfano, Proust aliamini kwamba "ni sitiari tu iwezayo kuupa mtindo namna fulani ya umilele", na Ezra Pound alitamka kuwa "ni bora kutunga taswira moja katika maisha yako yote kuliko kutunga majuzuu" (taz. Ullmann 1964: 174f.).

kuchanganuliwa kama vipengele vyovyote muhimu vya kifasihi. Kwa hiyo jambo la msingi linalochunguzwa hapa ni kama *sitiari ni mbinu ya msingi inayotumiwa na Kezilahabi katika kuchanuza maana katika mashairi yake*. Kwa hivi, lengo la makala ni la kiuelezi: kubainisha sitiari zilizomo katika mashairi teule na kuonyesha kuwa zina dhima kubwa kimaana. Ili kuibana makala katika mipaka iliyodhamiriwa, maandishi mengine ya Kezilahabi hayakuguswa. Kadhalika, ubainishaji umefanywa kwa kuzingatia nadharia na mbinu zilizoelezwa hapa chini, na si nyinginezo; na hakuna mjadala mrefu wa kinadharia wa sitiari.

## Nadharia

Uchunguzi juu ya sitiari una historia ndefu, na bibliografia ni ndefu (k.m. taz. Shibles 1971 na marejeleo katika Ortony 1993 na Gibbs 2008). Kadhalika ipo mitazamo mingi kuhusu kipengele hiki cha lugha – ya kiisimu, kifalsafa, kisaikolojia, kifasihi, na kadhalika.[2] Kulingana na malengo yetu, itatosha hapa kuelezea sitiari kwa mujibu wa (1) udhati wa sitiari, (2) muundo na aina za sitiari, na (3) tofauti baina ya sitiari na tamathali nyingine za semi.

### Udhati wa sitiari

Sitiari ni kipengele cha kisemantiki ambacho kwa kawaida hujumuishwa katika taswira au tamathali. Taswira ni kipengele chochote cha lugha kinachoibusha maono mahususi (au picha) akilini mwa mpokeaji yeyote wa fasihi kupitia kwenye milango yake ya fahamu hadi mtu huhisi kuwa anaona, anagusa, anaonja, anasikia au ananusa kitu kilichosawiriwa (taz. Friedman 1993). Maono au picha hiyo huweza kuibushwa na neno, fungu la maneno, matini ndogo katika matini kubwa (k.m. shairi zima au hadithi) au matini yoyote ndefu zaidi ya kifasihi au ya aina nyingine. Hata hivyo, ‘taswira’ ni dhana tata (taz. Ullmann 1964: 176f.): yaweza kurejelea maelezo tu ya kawaida (kiambo cha kawaida) au kiambo cha kitamathali. Ni katika maana ya pili ndipo taswira

[2] Inafaa itajwe kuwa, kihistoria, sitiari imeeleweka kwa namna tofautitofauti, na baadhi ya tofauti hizo bado zipo hadi leo. Kwa karne kadhaa (ya 16, 17, 18 huko Ulaya), wanafalsafa, wanalugha na wahakiki waliiona sitiari kuwa ni *pambo* lisiloweza kutumika katika kueleza mawazo mazito (taz. Richards 1936: 90 na Black 1962: 25). Mitazamo mingine ambayo imepata kushikiliwa na wataalamu ni: (i) *Mtazamo wa mbadala*: Mtazamo huu washikilia kuwa sitiari huweza kutumika badala ya kiambo cha kawaida – yaani sitiari haiongezi lolote kimaana. (ii) *Mtazamo wa ulinganisho*: Huu washikilia kuwa sitiari ni mlinganisho uliodokezwa – hausemwi kwa uwazi kama katika tashibiha. (iii) *Mtazamo wa mwingiliano*: Huu ulipendekezwa na Black (1962) kwa kutumia mawazo ya Richards (1936). Mtazamo huu washikilia kuwa maana ya sitiari hutokana na mwingiliano wa sifa za kitajwa na kifananishi. Richards (1936) na wanasemantiki kama Ullmann (1962, 1964) waliamini kuwa sitiari ni kanuni mahususi ya lugha inayotumika katika kuugawa, kuupanga na kuueleza ulimwengu. (iv) *Mtazamo wa upotoko wa kisemantiki*: Huu unaiona sitiari kuwa ni tokeo la uvunjaji wa kanuni za kisemantiki (taz. kwa mfano, Levin 1977). Mitazamo mingi inayowakilisha mikondo ya kisasa ya fikira juu ya sitiari yaweza kukutwa katika Ortony (1993) na ya kisasa zaidi katika Gibbs (2008).

huhusiana na sitiari. Kwani picha ya kitamathali yaweza kuibuliwa na kiambo cha kiisimu ambacho ni sitiari, tashibiha, tashihisi, taashira, majazi, au aina nyingine za tamathali.

Sitiari, kisemantiki, ni kipengele kinachohusisha "uhamishaji wa maana" kutoka kikoa kimoja kwenda kingine (taz. Leech 1969: 151-163; 1981: 214f.). Kwa tabia hii, sitiari huunganisha vikoa viwili vya maana. Muunganisho huu si kamili; kwani wakati huo huo kuna ukanushi wa muunganisho huo. Yaani usitiari wa kiambo kitokanacho na muunganisho huo unategemea upambanufu baina ya vipengele vyake. Kwa mfano, tusemapo "X ni kupe" tunaunganisha vikoa viwili vya 'binadamu' na 'wadudu', na kwamba maana (au sehemu ya maana) ya 'kupe' imehamishiwa kwenye 'binadamu'. Hata hivyo, bado X *si* kupe; na usitiari wa "X *ni* kupe" unategemea ukweli huo[3].

**Muundo na aina za sitiari**

Sitiari ya kawaida imeundwa kwa vipengele vitatu: *kitajwa, kifananishi* (au *kielezeo*), na *kiungo*[4]. Kwa mfano, tukitumia mfano wetu wa "X ni kupe", "X" ni "kitajwa" na "kupe" ni "kielezeo" au "kifananishi"; uhusiano baina ya vipengele hivi unajidhihirisha katika "kiungo" – ambacho ni mkusanyo wa "sifa" zinazoviunganisha vipengele viwili vya sitiari (taz. Richards 1936, Black 1962, Ullmann 1962 & 1964, Nowottny 2000, Semino & Steen 2008). Muundo wa sitiari unaodhihirika ni wa kipembe-tatu, unaohusisha vipengele hivi, kama ifuatavyo:



NYONYA = TEGEMEA WENGINE KWA MANUFAA

---

[3] Ricœur anajadili mtazamo huu wa sitiari na dhana yake ya sitiari kama kitenzi-shirikishi (na kikanushi chake) katika Ricœur (1979a, 1979b). Ricœur pia anaunga mkono msisitizo wa hivi karibuni kwamba ili kuielewa vizuri sitiari lazima tuikabili kama kipengele kilicho kwenye kiwango cha sentensi, na siyo neno (taz. makala zilizo katika Ortony 1993). Kinachosisitizwa siku hizi ni mtazamo unaoifikiria sitiari kuwa kwenye viwango vya sentensi na matini. Wanasemantiki kama Lakoff (1993, 2008) wanaichukulia sitiari (pamoja na taashira) kuwa vipengele vya msingi katika lugha katika mtazamo uitwao wa kiutambuzi.

[4] Richards (1936: 96-114) alipendekeza istilahi "tenor", "vehicle", na "ground" kuelezea muundo wa sitiari. Katika makala hii, tumetafsiri istilahi hizi kuwa *kitajwa*, *kifananishi*, na *kiungo*.

Uhusiano baina ya “kitajwa” na “kifananishi” unawakilishwa kwa sifa iliyobainishwa na “kiungo”, yaani “X” anahusiana na “kupe” kwa “kutegemea wengine kwa manufaa”.

Kwa mujibu wa muundo huo, zipo aina tatu za sitiari[5] ambazo msanii huweza kutumia. Aina ya kwanza ni *sitiari wazi*. Hapa kitajwa na kifananishi huelezwa kuwa ni sawa kwa kutumia kitenzi-shirikishi *ni*, yaani “Y ni Z” au Y=Z. Mifano ya aina hii ya sitiari ni mingi, k.m. “X ni kupe”, “maisha ni bahari tesi”, “maisha ni moshi”, na mingineyo. Aina ya pili ni *sitiari isiyo wazi (sitiari siwazi)* au *sitiari mkato*. Aina hii ni ile ambamo kitajwa na kielezeo vimetajwa lakini havina uhusiano wa usawa, k.m. “waya ngumu ya maisha” (*Nimechoka)*. Aina ya tatu ni ile ya *sitiari ishara*. Katika sitiari za aina hii, kitajwacho ni mifano tu, vitajwa havisemwi. Kwa kuwa vitajwa havisemwi, sitiari za aina hii huwa zina sawia mbili za maana: maana ya moja kwa moja, na ile ya sitiari ishara. Kwa hivi lazima zipatiwe tafsiri; kwa sababu hii, vitajwa vinaweza kutofautiana kulingana na masafa ya uvulivuli wa vifananishi. Mifano ya sitiari ishara ni: “nimening’inia” (ubeti 1, mstari 4, na mwinginemo), “kudondoka” (ub. 1, mst. 7, na mw.), “kichomi” (ub. 8, mst. 7) katika shairi la “Nimechoka”, Kezilahabi 1974: 34f.).

Muainisho mwingine ambao hutumika katika uchanganuzi wa sitiari ni ule unaotambua kuwepo kwa *sitiari sahili* (ile yenye kifananishi kimoja), *sitiari changamani* (yenye mifano miwili au zaidi ya miwili) na *sitiari pana* (ambayo huweza kuwa katika umbo la shairi au hadithi). Huu ni uainishaji wa “kimuundo” – kuanzia sitiari yenye *muundo sahili* hadi ile yenye *muundo changamani kabisa* (sitiari pana). Katika uchanganuzi wetu tutazitumia istilahi hizi kila inapohitajika.

**Tofauti baina ya sitiari na tamathali nyingine**

Katika uchanganuzi wetu tunapambanua sitiari na tamathali nyingine zinazokaribiana nayo. Hizi ni: *tashibiha, taashira* na *majazi*. Tashibiha hulinganisha vitu viwili kwa kutumia maneno *kama, kama kwamba* ama *mithili ya*. Mara nyingi hii ni rahisi kuitofautisha na sitiari kwa kuwa ulinganishi wake ni wa wazi tofauti na ule wa sitiari. Taashira huundika iwapo jina la kitu kinachohusiana na kitu fulani linatumika badala ya jina la kitu chenyewe, kwa kifananishi: *kiti cha enzi* → ufalme, *jembe* → ukulima, *ikulu* → raisi, n.k. Hapa *kiti cha enzi, jembe, ikulu* ni taashira. Uundaji wa majazi hutokea iwapo sehemu muhimu ya kitu inawakilisha kitu kizima. Mifano ni: *tanga* → chombo, *roho* → mtu, n.k., ambapo majazi ni *tanga* na *roho*. Tamathali nyingine, mathalani *tashihisi* na *mbalagha* zimejikita kwenye kanuni ya uhamishaji wa maana, ambayo ni msingi wa sitiari, na kwa hiyo zitachukuliwa kuwa ni sitiari. Tamathali nyingine zenye msingi wa kisitiari ni *isitiara, ishara* na *mbazi*. Tamathali zote hizi zinachangia sifa ya

---

[5] Aina hizi za sitiari zimejadiliwa na Perrine (1971, 1977). Inafaa tuseme kuwa hii si njia pekee ya kuichambua sitiari; hata hivyo inatosha kwa madhumuni yetu.

kuwa na sawia mbili za maana: maana ya moja kwa moja na maana isiyo ya moja kwa moja. Kwa mtazamo wa makala hii, tamathali hizi ni aina ya sitiari-ishara, inayojumuisha sitiari pana zote (taz. Leech 1969: 150-161).

Kwa kuzingatia misingi hiyo ya kinadharia, uchambuzi na uelezaji wa sitiari katika makala hii utafanywa kwa kuzingatia yafuatayo: kubainisha sitiari husika na kuelezea maana na muundo wa sitiari hizo na jinsi zinavyoshirikiana na sitiari nyingine.

## Sitiari katika *Kichomi*

Uchambuzi wetu wa sitiari utajikita kwenye dhamira tatu: maana ya maisha, dhuluma ya kikoloni, na hali ya sasa ya Afrika. Tumefuata mtazamo wa kidhamira ili kurahisisha uwasilishaji.

### Maana ya maisha

Dhamira ya "maana ya maisha" ni miongoni mwa mambo ambayo Kezilahabi ameshughulika nayo. Inajitokeza zaidi katika mashairi yafuatayo: "Nimechoka" (Kezilahabi 1974: 34f.), "Upepo wa Wakati" (hapohapo: 4), "Mwamba Ziwani" (6), "Fungueni Mlango" (23), "Dhamiri Yangu" (36), "Kisu Mkononi" (13). Tutayachambua kufuata mpangilio huo, mtawalia.

Katika shairi "Nimechoka" (uk. 34f.), mshairi anatamka kwa uzito na kwa sitiari changamani kuliko mahali pengine falsafa yake ya maisha. Mashairi mengine ama yanatoa nyongeza kwa kile kilichokwishasemwa au yanasisitiza kipengele fulani cha falsafa inayotolewa katika shairi hili. Tutachambua sitiari muhimu zinazojitokeza kuanzia ubeti wa kwanza hadi wa mwisho.

Mwanzoni mwa shairi tunamkuta mshairi amepandishwa kwenye "waya [...] ngumu ya maisha" ambayo "ncha" zake hajui "zilipofungwa":

> Nilivyofikishwa hapa, na juu kupandishwa,
> Na kwa hila gani, au, zilipofungwa
> Ncha za waya hii ngumu ya maisha, sijui.
> ("Nimechoka", uk. 34, ub. 1, mst. 1-3)

Sitiari inayovuta udadisi wetu hapa ni "waya ngumu ya maisha". 'Waya ngumu' inahusianaje na maisha? 'Waya ngumu' huweza kukata au kuumiza. Kwa hivi, 'waya ngumu' inahusiana na maisha kwa sifa hii ya 'kukata na kuumiza'. Matatizo ya kimaisha pia huwaumiza watu. Kadhalika, 'waya ngumu' inahusiana na maisha kwa vile ncha za waya hii hazijulikani zilipofungwa. Yaani chanzo na mwisho wa maisha havijulikani. Muundo wa sitiari hii utakuwa kama ifuatavyo:

SITIARI KATIKA *KICHOMI*




Mshairi anaendelea kutuambia:

> Lakini najiona nimening'inia kama ndege
> Aliyenaswa na mtego wa mtoto mdogo.
> (hapohapo, mst. 4-5)

Sitiari ya "kunaswa na mtego wa mtoto mdogo" inazidi kueleza hali ya mshairi. Mtego wa mtoto mdogo si "mtego kitu". Mtoto hutega mitego kama mojawapo ya michezo yake ya kila siku, michezo ya kitoto. Mshairi anapolinganisha hali yake ya "kuning'inia kwenye waya" na "hali ya ndege aliyenaswa na mtego wa mtoto mdogo" anazidi kusisitiza kuwa maisha "huwanasa watu" bila wao kujua, bila hiari, kama ndege anaswaye na mtego wa mtoto mdogo asivyojua na asivyokuwa na hiari katika hili. Sitiari hii inao muundo ufuatao:




Ifahamike kuwa sitiari "ndege kwenye mtego wa mtoto mdogo" inatumika kama kifananishi kushadidia hali mbaya ya "mtu anayening'inia kwenye waya" (kitajwa).

Katika hali hii, kwa nini msemaji (mshairi) “asidondoke” kutoka kwenye “waya ngumu ya maisha”? Japo anatambua wazi kuwa yeye siyo “ndege” bali mtu mwenye akili anaogopa kudondoka:

> [...] ninaogopa chini yangu naona miti
> Iliyochongwa ikifuata usawa wa waya hii,
> Ikingoja kwa hamu, kama mshikaki kunichoma,
> Kunitoboa na kufurahia kimya kimya
> Uzuri wa kupita katika mwili mwororo wa binadamu.
> (hapo hapo, ub. 2, mst. 1-5)

Hawezi kuondoka kutoka kwenye “waya ngumu” ya maisha kwa vile mara adondokapo tu atamalizwa na miti iliochongwa kufuata usawa wa waya (yaani, vitimbo). “Waya ngumu” na “vitimbo” vimepangwa kwenye usawa mmoja, kimoja juu (waya) na kingine chini (vitimbo). Vitu hivi vina kazi na matokeo tofauti: “kuning’inia kwenye waya” maana yake ni “kuishi” na “kudondoka kwenye vitimbo” maana yake ni kinyume kabisa: “kufa”. Katika hali hii, mshairi hana hiari ila kuendelea kushikilia waya ngumu ya maisha kwa nguvu asije akaanguka.

Kuendelea kushikilia “waya ngumu” ya maisha kumemuathiri sana. Maisha yamekwishamu-umiza (“waya imekwishanikata vidole”, ub. 3, mst. 1) na wala maumivu hayo hawezi kuyaondoa (“Damu imetiririka hadi kwapani, kujipangusa siwezi”, mst. 2). Hivyo, kuishi kumemchosha na sura yake inaonyesha “alama za uchovu” (mst. 4). Hizi “alama za uchovu” zinaweza kuwa ama alama zionyeshazo masumbuko aliyopata.

Sitiari inayojitokeza sana hapa ni ile ya damu.

> [...] waya imekwishanikata vidole.
> Damu imetitirika hadi kwapani, kujipangusa siwezi.
> (ub. 3, mst. 3-4)

Sitiari ya damu inao muundo ufuatao:



Sitiari hii ya damu inawiana na sitiari nyingine tunayokutana nayo katika ubeti ufuatao; sitiari ya machozi:

> Machozi yananitoka; kuyapangusa siwezi.
> (ub. 4, mst. 4)

Mtu anapokatwa na damu ikamtoka kwa wingi ikatiririka hadi kwapani asiweze kuipangusa yamkini atalia sana kwa uchungu wa yale yaliyompata. Hivyo machozi ni tokeo la kukatwa na kutokwa na damu. Yanawakilisha uchungu na huzuni iliyo ndani. Muundo wa sitiari ya machozi yasiyopangusika unafanana na muundo wa sitiari ya damu isiyopangusika:




Katika ubeti wa tano mshairi anatupeleka kwenye ulimwengu wa “vichwa vyeupe” au mafuvu. Mafuvu haya yanazuka kati ya vitimbo kutoka ardhini.

> Kati ya vitimbo, vichwa vyeupe vinazuka ardhini.
> (hapohapo, uk. 35, ub. 5, mst. 1)

“Vichwa vyeupe” vinawakilisha watu ambao wameshapitia katika maisha na kufa; ni sitiari-ishara ya umauti. Muundo wa sitiari hii ni huu ufuatao:



Kiungo “Utovu wa uhai” kinatofautisha “vichwa vyeupe” na binadamu anaye“ning’inia” (hapo juu). Kwa kuwa binadamu ana uhai (ana hisi, akikatwa anatoka damu, n.k.), ataendelea kupata maumivu ya uhai huo.

Baada ya sauti ya baba yake ambaye yumo miongoni mwa vichwa vyeupe kumuasa aendelee kushikilia waya (kuishi), asikate tamaa, asitegemee kushangiliwa au kusaidiwa na kwamba wakati utimupo atadondoka (atakufa), mshairi anaanza kutambua nini maana ya maisha:

> [...] pole pole ninaanza kutabasamu.
> Sijafikia hatua ya kucheka; maana nimechoka,
> Kichomi kimenipata na sijadondoka.
> (ub. 8, mst. 5-8)

“Tabasamu” la mshairi ni la kiishara: linaashiria kuanza kwa utambuzi wake juu ya maana ya maisha. Sitiari muhimu hapa ni ile ya “kichomi”. “Kichomi” hapa kina maana mbili: maumivu makali, na kitu kinachochoma au kinachotumika kuchomea (yaani kinachosababisha maumivu, damu, machozi, n.k.). Mshairi anataka kutuambia kuwa “maisha ni kichomi”. Muundo wa sitiari hii uko hivi:




Katika muundo huu, uhusiano baina ya “kichomi” na “maisha” uko wazi. Mtu achomwapo na kichomi (yaani silaha) hupata maumivu makali. Damu humtoka, na wakati mwingine huweza kutokwa hata na machozi. Ikiwa kichomi hiki (kisu, mkuki, umambo, n.k.) kimempata mahali pabaya sana (kwa mfano, moyo, kifua, n.k.) na hakupata matibabu anayofaa, mtu huyu huweza kufa. Mshairi anatuambia kuwa maisha yanavyo “vichomi” vyake. Yamejaa dhiki, matatizo na mashaka mengi ambayo huwaumiza watu, magonjwa aina aina, misiba aina aina; migogoro aina aina ambayo huacha alama zake kwenye maisha ya watu binafsi, n.k. Kichomi si silaha tu, bali pia ni maumivu yatokanayo na utumizi wa silaha hiyo.

## SITIARI KATIKA *KICHOMI*

Sitiari ya kichomi haifanyi kazi peke yake. Inashirikiana na taswira nyingine ambayo lazima tuizingatie; nayo ni picha ya upweke. Taswira hii imechorwa kwa kuunganisha sitiari kadhaa. Kwanza, ipo sitiari ya mtu aliyening'inia kwenye waya ya maisha peke yake. Pili, ipo picha ya watu wanaosali bila kujali malalamiko ya mtu aliyening'inia. Tatu, yapo "mafuvu" ambayo vile vile hayamjali mtu anayening'inia. Mtu huyu anaonekana mpweke kabisa. Lazima apambane na kichomi cha maisha peke yake, pasipo msaada.

Kutokana na mjadala huu wa sitiari za shairi hili, tunaweza kutoa mahitimisho yafuatayo:

(1) Shairi hili limeundwa na mwingiliano na uchangamani wa sitiari kadhaa
(a) waya ngumu; (b) mtu anayening'inia kwenye waya ngumu
(c) vitimbo; (d) vichwa vyeupe; (e) kichomi

(2) Sitiari za msingi (yaani zinazojitokeza tangu mwanzo hadi mwisho) ni "waya ngumu", "mtu anayening'inia", "vitimbo", na "kichomi".

(3) Kutokana na hayo, tunaweza kusema kuwa shairi hili limeundwa na sitiari changamani juu ya maisha.

Mtazamo wa maisha unaojitokeza katika sitiari tulizoziangalia katika shairi "Nimechoka" unajitokeza vile vile katika mashairi mengine. Sitiari changamani ya maisha tunayopata katika shairi hilo inazidi kutajirishwa na sitiari nyingine kuhusu maisha.

Katika shairi "Upepo wa Wakati" (uk. 4), tunapatiwa picha nyingine ya maisha. Picha hii ni ya ziwa lililojaa mawimbi yacharukayo kwa kupanda na kushuka, na kujisukasuka:

Nikatazama chini ziwani, siku
Ya dhoruba. Halafu niliona mawimbi
Yakipanda na kushuka. Yakivimba,
Yakiviringika, yakigongana na kutoa povu
Kama fahari wehu katika bonde lisomajani.
Yalivyotengenezwa!
Yalivyofifia na kuanza tena!
Kamwe sikuona.
Lakini niliyaona yakishuka ka nguvu
Na kupanda haraka, yakisukumwa
Na upepo wa Magharibi na Mashariki.

Hivyo ndivyo ulimwengu ulivyo.
Na hivyo maisha ya binadamu.
("Upepo wa Wakati", uk. 4, ub. 1, mst. 3-13; ub. 2, mst. 1-2)

Picha ya maisha tunayopata hapa ni ile ya maisha yaliyojaa “mawimbi” (ub. 1, mst. 4) ambayo hufifia na kuanza tena. Muundo wa sitiari hii ya mawimbi ni huu ufuatao:




Sitiari changamani ya maisha tuipatayo katika “Nimechoka” inawiana na sitiari ya mawimbi kwa namna fulani. Sitiari ya ‘maisha ni kichomi’ inashughulika na maisha ya mtu binafsi (mshairi), sitiari ya ‘maisha ni mawimbi yapandayo na kushuka’ inashughulika na maisha kwenye kiwango binafsi na cha kijamii. Kama ambavyo maisha ya mtu binafsi huonesha “kupanda na kushuka” (kufanikiwa na kinyume chake), hata maisha ya jamii hudhihirisha “kupanda na kushuka”. Mfano wa wazi ni kuwa jamii au nchi inaweza kupata mafanikio makubwa katika kipindi fulani na katika kipindi kingine mafanikio hayo yakatoweka kwa sababu mbalimbali.

Katika shairi jingine, “Mwamba Ziwani” (uk. 6), mtazamo huu wa kuyaona maisha kama kitu kilichojaa misukosuko na kwamba mtu akiwa hai husumbuliwa na misukosuko hiyo hadi afe, unaendelezwa. Mtazamo huu unaendelezwa katika sitiari changamani ambamo sitiari mbili zinazotofautiana na kupingana, zinapambanishwa ili kuutoa wazi msimamo wa mwandishi. Sitiari hizi ni ‘mwamba’ ulio ziwani na ‘mtu aliye melini’. Mshairi anaufanya mwamba uzungumze:

> “[...] mimi nimetulia,
> Sina wasiwasi ingawa naonekana mjinga.
> Mawimbi yananigusa na kuvunjika
> Kama upanga wa mauaji ushindwavyo kwa roho.
> Mimi ni imara na sihamishiki.
> Na mtu mwovu siumiziki.”
> (“Mwamba Ziwani”, uk. 6, [halina beti,] mst. 5-10)

Hapa tunaelezwa kuwa mwamba huu ambao hauishi, umetulia, hauna wasiwasi, “mawimbi” (mst. 7; misukosuko ya maisha) hayauathiri kwa njia yoyote. Picha hii inapambanishwa na picha ya ‘mtu aliye melini’ (meli hii ni ya kisitiari: ‘meli ya maisha’ inayorakibu ‘ziwa la maisha’).

Hapa ndipo nilipo, melini, mtu mwovu,
Na mwenye wasiwasi
Nikisukumwa na mawimbi,
Nikitetemeshwa na mapaja ya huyu msichana
Mbichi karibu nami. [...]
(hapohapo, mst. 12-16)

Mtu katika ‘meli ziwani’, tofauti na “mwamba ziwani” (kichwa cha shairi), ni mwovu, mwenye wasiwasi, anayesumbuliwa na mawimbi ya maisha (misukosuko) na tamaa aina aina (k.m. kutetemeshwa na msichana). Baada ya kupatiwa picha hizi mbili za mambo yanayotofautiana, tunaelezwa:

[...] Lakini ule mwamba,
Ule mwamba ulikuwa umekufa.
Wakati wote niishipo sitaweza, nao kufanana.
Nitakapokufa kama huo mwamba,
Huo mwamba nitaushabihi.
(mst. 16-20)

Wazo linaloelezwa hapa ni kuwa mshairi akiwa bado anaishi hawezi kufanana na mwamba ziwani, hawezi kupata utulivu, na uthabiti ambao mwamba unao. Akiwa bado angali kwenye meli ya maisha, atazidi kusumbuliwa na wasiwasi, tamaa, na mawimbi (misukosuko) ya maisha. Kwa ufupi, anataka kutuambia kuwa utulivu mtu huupata pindi tu anapokufa. Maisha hayana utulivu, bali wasiwasi, tamaa aina aina na mawimbi yasiyotulia. Kwa kuzipambanisha sitiari hizi mbili mwandishi anasisitiza wazo lake ambalo limeshagusiwa huko nyuma kwamba maisha ni madhilifu na madhaifu, yenye migogoro isiyokwisha.

Sitiari ya “mwamba ziwani” ni sitiari-ishara; inawakilisha kitu chochote kisicho hai; hakisumbuliwi na “mawimbi”. Muundo wake ni rahisi:

Kitajwa — Kifananishi
KITU KISICHO HAI — MWAMBA ZIWANI



Kiungo
UTOVU WA HISI; MISUKOSUKO

Wakati “mwamba ziwani” (yaani kitu chochote kisicho hai) hauhangaishwi na misukosuko ya maisha, mtu akiwa katika ‘meli ziwani’ anahangaishwa na misukosuko mbalimbali. Muundo wa sitiari hii ni huu ufuatao:




Mtu akiwa bado yu hai, ataendelea kusumbuliwa na misukosuko kama ‘meli ziwani’ inavyo-sumbuliwa na misukosuko.

Katika shairi jingine “Kisu Mkononi” (uk. 13) tunaelezwa jinsi madhila na mashaka ya maisha yanavyokatisha tamaa na kumsukuma mshairi atake kujiua kwa kisu, lakini hatimaye anaamua kutojiua kwa vile hii haitasaidia. Mshairi anayalinganisha maisha na mtelemko mkali ambao haujui mwisho wake na yeye kama gurudumu ambalo halina budi kuviringika kwenye mtelemko huu.

> Wakati miaka inaibwa mmoja mmoja,
> Kurudi nyuma, kusimama, kupunguza mwendo
> Siwezi, kama gurudumu nitajiviringisha.
> Mtelemko mkali huu.
> Lini na wapi mwisho sijui:
> (“Kisu Mkononi”, uk. 13, ub. 1, mst. 1-5)

Gurudumu likiwa kwenye mtelemko mkali halina hiari bali kutelemka tu pasipo kujua mwisho wa mtelemko. Katika maisha hali ni kama hiyo: mtu anasukumwa tu kila siku, anaendelea kuishi na mambo mengi yanatendeka bila yeye kupenda na wala kujua mwisho wa maisha yenyewe. Na mshairi anakiri kuwa hana hiari bali kuendelea ku“jiviringisha” (mst. 3) kwenye mtelemko huo mkali. Muundo wa sitiari ya gurudumu mtelemkoni ni huu:



Mshairi anaendelea kutuambia:

> Mbele chui mweusi, nyuma mwanga
> Nionako kwa huzuni vifurushi maelfu vya dhambi.
> (hapohapo, ub. 2, mst. 1-2)

Maisha ya nyuma ndiyo anayoyajua na yanakatisha tamaa kwa vile hakuna lolote zuri alionalo huko. Maisha ya mbele mshairi hayajui na ni ya hatari: *ni* "chui mweusi" (mst. 1). Sitiari hii ya "chui mweusi" inazidi kusisitiza hatari iliyo katika maisha. Sitiari hii inaweza kuwakilishwa hivi:

Kitajwa — Kifananishi

MAISHA YA MBELE — CHUI MWEUSI



Kiungo

HATARI ILIYOFICHIKA

Katika shairi jingine, "Fungueni Mlango" (uk. 23), mshairi anayaona maisha kama kifungo kilichojaa upweke:

> Hewa kunikosa
> Na jasho kunitoka ndani ya chumba
> Kwa upweke
> Ninajiona nimefungiwa.
> ("Fungueni Mlango", uk. 23, ub. 1, mst. 1-4)

Katika kifungo hiki, mshairi anatapatapa akipiga kelele ili watu wamfungulie:

> Ninapiga kelele kama
> Ng'ombe machinjioni:
> Fungueni mlango!
> Mlango fungueni!
> Lakini mwanadamu hatanifungulia.
> (hapohapo, ub. 2, mst. 2-6)

Muundo wa sitiari hii unaweza kuwakilishwa hivi:




Sitiari hii ya ‘kifungo’ inaendelezwa katika shairi jingine “Dhamiri Yangu” (uk. 36). Hapa mshairi anajiona amefungwa kwa ‘kamba ya dhamiri/dhamira’ “kwenye mti wa utu”:

> Dhamiri imenifunga shingoni.
> Nami kama mbuzi nimefungwa
> Kwenye mti wa utu. Kamba ni fupi
> (“Dhamiri Yangu”, uk. 36, ub. 1, mst. 1-3)

Mshairi anakubaliana na kifungo hicho, kwani

> Mbuzi wa kamba alipofunguliwa, mashamba
> Aliharibu na mbwa aliuma watu.
> (hapohapo, ub. 3, mst. 3-4)

Sasa tutahitimisha juu ya sitiari tulizozizungumzia. Katika uchunguzi wetu, jambo linalojitokeza dhahiri ni kuwa sitiari zote tulizozichunguza zinaongelea kitu kimoja tu: maisha. Kila sitiari inaongelea kipengele fulani cha maisha, ingawa sitiari zingine zimechangamana kuliko zingine. Kadhalika, mawazo na mtazamo unaojitokeza katika sitiari zote unaeleza na kusisitiza msimamo thabiti wa mwandishi juu ya maisha. Kwa hiyo, sitiari zote hizo zinaweza kukusanywa katika sitiari changamani moja tu juu ya maisha.



Uchangamani wa sitiari hii tuliyoipata kwa kuchunguza mashairi sita katika *Kichomi* ("Nimechoka", "Upepo wa Wakati", "Mamba Ziwani", "Fungueni Mlango", "Dhamiri Yangu" na "Kisu Mkononi") unadhihirishwa na vipengele viwili vya muundo wake: vifananishi na kiungo. Vipengele hivi ni vingi. Wingi wa vifananishi na viungo unaeleza na kusisitiza uchangamani wa kitajwa. Na hii ndiyo picha inayojitokeza kuhusu maisha kama yanavyoonwa na mshairi.

**Udhalimu wa kikoloni**

Eneo jingine la kidhamira linalozingatiwa na *Kichomi* ni udhalimu wa kikoloni. Tumeteua shairi la "Hadithi ya Mzee" (uk. 69-72) kuwakilisha dhamira hii.

Katika shairi hili lenye muundo wa kimasimulizi mshairi ameunda sitiari madhubuti inayowiana na matendo ya wakoloni: sitiari ya nzige. Wakoloni ndio nzige. Tangu mwanzo wa shairi hili hadi mwisho tunaelezwa kwa kifupi yaliyotokea tangu wakoloni wa Kijerumani kuja hadi uhuru kupatikana.

Habari za kuja kwa "nzige" (hapohapo, ub. 1, mst. 8 na mwinginemo) zilienea bara kutoka pwani. Habari hizi zilisema kuwa "nzige" hawa hula kila wakati na kuangamiza majani yote mitini. Walikuwa "walafi kama fisi" (ub. 5, mst. 4) na walizungumza "lugha isiyoeleweka" (hapohapo, mst. 6). Baadaye habari zilienea bara kuwa nzige wameshaangamiza mimea yote ya pwani na sasa wanaelekea bara. Tena habari nyingine za kutisha zikafika:

> Huo huo mwaka huo
> Tukasikia vifo na njaa
> Tukasikia kwa huzuni
> Kwamba kulikuwa na vita
> Kati ya nzige na wanadamu
> Kwamba nzige walishinda.
> Na damu ya wanadamu
> Nyingi chini ilimwagika.
> ("Hadithi ya Mzee", uk. 70, ub. 8, mst. 1-8 [ubeti mzima])

Watu wakajiandaa kwa vita ili wajihami kutokana na baa hili. Wakatengeneza mikuki, ngao na kadhalika. Lakini haya yote hayakufaa kitu. Siku moja mchana nzige walikuja na kitua juu ya mimea na kuanza kuiangamiza.

> Mikuki haikufaa
> Mishale haikufaa
> Maana silaha yao
> Ilikuwa ni kupumbaza

> Miguu ilikufa ganzi
> Sauti zilitukauka
> Tukabakia kuduwaa
> Kuwatazama wanyonyaji.
> (hapohapo, uk. 70, ub. 13: mst. 1-8 [ubeti mzima])

Nzige hao wa kwanza hawakukaa sana (yaani Wajerumani). Baada ya kuangamiza mimea yote waliondoka na watu wakaanza kuwa na matumaini mapya. Lakini huo haukuwa mwisho wa hadithi ya nzige; nzige wengine walikuja (yaani Waingereza).

Punde kulitokea zinduko la kupigania uhuru. “Nzige” wakafukuzwa. Sitiari hii inao muundo ufuatao:




Mshairi, kwa kutumia sitiari ya nzige ili kuvieleza vitendo ya wakoloni, amefaulu kuonyesha “unzige” wao. Wakoloni hawaitwi “binadamu”; katika shairi zima wanaitwa “nzige”. Katika shairi zima tunaona “nzige” wanapambana na “binadamu”. Mtazamo wa mshairi juu ya wakoloni unajitokeza wazi. Mshairi, katika shairi hili, anapinga kwa uwazi kabisa ukoloni wa aina yoyote, si katika bara la Afrika tu bali mahali popote duniani.

**Hali ya sasa ya Afrika**

Kundi jingine la sitiari tutakazoeleza ni zile zinazohusiana na hali ya sasa ya Afrika, kisiasa, kijamii na kiuchumi. Mashairi yanayohusika hapa ni “Hadithi ya Mzee” (uk. 69-72), “Afrika na Watu Wake” (uk. 19), “Kumbe” (uk. 37), na “Namagondo” (uk. 67f.).

Tutaanza na shairi la “Hadithi ya Mzee” (uk. 69-72). Mbali na kuelezea madhara ya ukoloni, shairi hili linaeleza madhara ya tabaka la mabwanyenye lililoibuka Afrika baada ya uhuru. Tabaka hili liliiga utamaduni wa kinyonyaji wa “nzige”:

## SITIARI KATIKA *KICHOMI*

Kulikuja kundi jingine
Tena kubwa zaidi
Hili likakaa
Likatufundisha lugha
Lugha hiyo ya nzige
Wanadamu tukaimudu
Tukawaona wazuri.

Wakatufunza na kula
Kula kama nzige
Yaani bila kushiba.
Halafu maajabu yakatokea
Tukaotesha mbawa
Tukaanza kuruka
Kuruka huko hewani
Kimawazo kama nzige.
(“Hadithi ya Mzee”, uk. 71, ub. 16, mst. 2-8; ub. 17, mst. 1-8 [ubeti mzima])

Kundi la nzige liliwafunza watu lugha yao, na watu wakaimudu na wakaanza kuwapenda. Wakafunzwa pia kula “bila kushiba” (yaani kunyonya; ub. 17, mst. 3). Kwa vile walijua lugha ya nzige, na pia kujua kula bila kushiba, wakawa wamefanana na nzige, wakaotesha mbawa na kuanza “kuruka [...] kimawazo kama nzige” (hapohapo, mst. 7f.). Hawa wanaoongelewa ni ‘wazungu weusi’ ambao walikuwa wamezongwa kwenye kasumba ya kikoloni na ambao walirithi mwenendo wa kikoloni wa ulafi wa kinyonyaji. Sitiari inayojitokeza hapa ni ya “lugha [...] ya nzige” (ub. 16, ub. 6):



Licha ya kueleza tatizo la tabaka la kibwanyenye, mshairi anaendelea kusawiri hali ya sasa ya Afrika katika shairi la “Afrika na Watu Wake” (uk. 19).

Katika shairi hili, mshairi analiona bara la Afrika kama bara lenye ndwele mbaya sana. Ndwele hii imelifanya liwe dhaifu sana hata lisiweze kuamka na kutembea huku likijitegemea:

> Mimi ninaona mgonjwa
> Bado amelala kitandani.
> Kaa hatutamtoa miiba iliyobaki
> Mgonjwa hataweka miguu yake chini
> Ili kutembea bila kujiegemeza.
> (“Afrika na Watu Wake”, uk. 19, ub. 1, mst. 1-5 [ubeti mzima])

Sitiari hii ya ndwele ndiyo inayotawala shairi zima na kimuundo tunaweza kuiwakilisha hivi:




Ndwele mbaya ambayo inaikabili Afrika ni hali ya kutojitegemea katika nyanja zote: kisiasa, kiuchumi, kitamaduni.

Katika shairi jingine “Kumbe” (uk. 37) mshairi anazungumzia ubovu wa mfumo wa elimu wa kikoloni. Anatumia sitiari dhahiri mbili katika shairi hili. Sitiari ya kwanza inahusu elimu ya kikoloni:

> Kwamba elimu walotupa wale wakoloni
> Kama suruali iliyopasuka matakoni,
> Kweli kama ng’ombe walioshtushwa
> Na siafu, tumetambua dhahiri.
> (“Kumbe”, uk. 37, ub. 1, mst. 1-4 [ubeti mzima])

## SITIARI KATIKA *KICHOMI*

Sitiari inayojitokeza katika ubeti huu inao muundo ufuatao:




Sitiari ya pili katika shairi hili inazingatia hali ya kimsiba iliyoikuta Afrika nzima:

> Sikilizeni. Simba aliyeumizwa,
> Bila haya alijikokota kwa unyonge
> Mpaka nyumbani, vidonda vikalambwa
> Vikapona kwa mate ya nyumbani
> (hapohapo, ub. 4, mst. 1-4 [ubeti mzima])

Hapa kuna sitiari tatu: "simba aliyeumizwa" (mst. 1), "vidonda" (mst. 3), na "mate ya nyumbani" (mst. 4). Muundo wa sitiari ya kwanza ni huu ufuatao:




Sitiari ya vidonda inaelezea maafa au madhara ambayo Afrika imeyapata kutokana na ukoloni (na hata kutokana na unyonyaji ulioendelea baada ya ukoloni). Muundo wake ni rahisi:

## KULIKOYELA KAHIGI




Sitiari ya mwisho ya “mate ya nyumbani” inaweza kutafsiriwa kuwa ‘dawa’ halisi ya kurejea kwenye misingi ya kijadi ya utu kama ile iliyoelezwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika siasa yake ya *Ujamaa* (Nyerere 1968). Ni sitiari ya mate ya nyumbani ni ya kiishara. Muundo wa sitiari hii ni huu ufuatao:




Misingi ya kijadi ya Mwalimu Nyerere ilijikita kwenye udugu wa kusaidiana, kushirikiana na kutendeana kwa usawa katika nyanja zote. Lengo lilikuwa kuinua watu wote ili waendelee kwa pamoja.

Katika shairi jingine, “Namagondo” (uk. 67f.), mshairi anatueleza juu ya kuharibika kwa maisha katika kijiji chake alimozaliwa. Zamani maisha ya kijiji yalistawi sana kiuchumi, kijamii na kitamaduni, lakini siku hizi ustawi huo haupo tena. Maisha hayo yaliharibiwa na mfumo wa kikoloni uliofanya kaya zivunjike, watu kutawanyika na uchumi wa kijiji kuharibika. Ni kilio cha mshairi juu ya msiba huo ambao, katika kijiji chake, ulileta na wakoloni. Kiishara, shairi hili halihusu kijiji cha mshairi tu. Linahusu msiba ulioipata Afrika (au mahali popote ambapo kipindi cha ustawi kinafuatwa na kipindi cha uhaba na dhiki.)

## SITIARI KATIKA *KICHOMI*

Katika shairi hili tunachorewa sitiari mbili zinazoeleza hali mbili tofauti: hali ya ustawi iliyokwisha pita na hali halisi ya leo iliyojaa uhaba. Muundo wa sitiari ihusuyo hali ya ustawi wa maisha yaliyopita ni huu:




Sambamba na picha hiyo tunapatiwa sitiari nyingine inayoeleza hali tofauti kabisa:




Sitiari hizi mbili zinajitokeza katika shairi katika uhusiano wa kupingana. Katika sitiari ya kwanza, kile kitajwa, kiungo, na vifananishi ni kinyume cha yale yaliyo katika sitiari ya pili. Mkinzano uliopo baina ya sitiari hizi mbili ndio unaolishika shairi pamoja.

Baada ya kuzichunguza sitiari katika mashairi hayo tunagundua jambo moja: zote (kuondoa ile ihusuyo hali ya ustawi iliyopita) zinahusu hali halisi ya Afrika ya leo. Hivyo, ingawa kijuujuu ni sitiari tofauti, tunapochunguza vifananishi na viungo vya sitiari hizi tunagundua kuwa

zinaongelea hali ile ile kwa namna mbalimbali. Na hali hii ni kwamba Afrika inayo matatizo ya kijamii yaliyotokana na wakoloni yanayoidhoofisha. Kutokana na sitiari hizo, tunaweza kuunda sitiari moja yenye muundo ufuatao:




Sitiari tulizozijadili hapa juu zina nguvu ya kihisia inayojitokeza kidhahiri. Mshairi katika sitiari zote tulizozichanganua pamoja na kuunda sitiari changamani moja, amefaulu kueleza wazo lake pamoja na kueleza uchungu wake juu ya msiba wa Afrika. Pengine ingefaa tuvipitie vifananishi alivyotumia ili wazo hili lieleweke vizuri. Mshairi anatumia vifananishi kama ndwele ("Afrika na Watu Wake"), simba aliyeumizwa ("Kumbe"), makaburi ("Namagondo"), na uhaba wa mazao (hapohapo). Kifananishi cha ndwele kinasisitiza udhaifu wa Afrika, na udhaifu huu unavuta shufaka na huruma. Mtu mgonjwa huvuta huruma ya wenzake, nao hujitahidi kadiri ya uwezo wao kumtafutia dawa ili apate nafuu. Mshairi anatumia kifananishi hiki ili avute hisia za wote wenye huba na Afrika watafute dawa ili bara lipate nafuu. Kifananishi cha simba aliyeumizwa, licha ya kusisitiza udhaifu wa Afrika, inasisitiza pia dhuluma ambayo Afrika ilifanyiwa ('iliumizwa'); na nguvu yake ya kihisia siyo ya kutia huruma tu, bali pia uchungu na ghadhabu kwa ajili ya dhuluma iliyotendwa. Kifananishi cha makaburi kinasisitiza kuwa Afrika ya zamani imeshakufa na kuzikwa na sitiari inavuta hisia za kumbukizi za kupotelewa na kitu cha thamani. Kifananishi hiki pia kinaibua hisia za hofu za ukiwa na utovu wa uhai. Na kwa kuibua hisia hizi kinasisitiza uzito wa msiba ulioikuta Afrika. Kifananishi cha uhaba wa mazao kinasisitiza upungufu uliopo katika nyanja zote za maisha katika bara hili. Afrika ina njaa – njaa ya uhuru, njaa ya chakula, na njaa nyinginezo.

Na vifananishi vyote hivi kwa pamoja vinatoa picha ambayo inaibua hisia za kizalendo kwa Mwafrika yeyote aliye tayari kushiriki katika kuiponya ndwele inayolikabili bara.

## Hitimisho

Uchambuzi katika makala hii unaonyesha kuwa Kezilahabi alizingatia kwa kiasi kikubwa kauli yake kwamba “Jambo ninalojali sana katika ushairi ni utumiaji wa picha au taswira” (*Kichomi*, uk. xiv). Katika uchambuzi tuliofanya tumejikita kwenye aina moja tu ya taswira, yaani sitiari. Uchambuzi wetu umeonesha kuwa Kezilahabi alitumia mbinu ya sitiari kama mbinu muhimu kabisa ya kisanaa katika kusawiri mawazo na hisia zake kuhusu maana ya maisha, madhara ya ukoloni, na hali halisi ya Afrika wakati alipokuwa akiandika mashairi yake (na hata hivi leo, kwa sababu maisha hayajabadilika sana).

Kwa kutumia nadharia ya sitiari iliyojikita kwenye nadharia ya maana katika kuzichambua sitiari za *Kichomi* tumethibitisha mambo kadhaa.

Kwanza, tumeona kuwa sitiari ni chombo thabiti cha mawazo na mtazamo wa kifalsafa wa mshairi. Kadhalika, sitiari ni chombo cha kihisia. Mambo haya mawili, wazo na hisia, ni pande mbili za sitiari zisizoachana.

Jambo jingine tulililoliona ni kuwa sitiari zinaweza kutumia mifano tofauti lakini kimsingi zinalozungumzia ni jambo moja. Tumeweza kuonyesha kuwa sitiari hizi zinaweza kuunganishwa pamoja na kuunda sitiari changamani moja.

Jambo la mwisho ni kuwa tunatumaini tumeonesha kuwa mbinu ya kuchanganua sitiari kwa mkabala wa kisemantiki (kama uliotumika humu) ni njia mojawapo yenye manufaa katika uchambuzi wa matini za kifasihi. Kwa kuzingatia muundo wa sitiari (wenye vipengele vitatu: kitajwa, kifananishi na kiungo), uchambuzi huu huchambua sitiari za kifasihi kwa uwazi kwa kubainisha maana na hisia vinavyobebwa na sitiari hizo.

## Marejeleo

Black, Max. 1962. *Models and Metaphors*. *Studies in Language and Philosophy*. Ithaca: Cornell UP.

Friedman, Norman. 1993. Imagery. Alex Preminger & Terry V. F. Brogan (wah.). uk. 559-566.

Gibbs, Raymond W. (mh.) 2008. *The Cambridge Handbook of Metaphor and Thought*. Cambridge: Cambridge UP.

Kahigi, Kulikoyela. 1976. Kezilahabi: Mwandishi wa Riwaya na Mshairi. Kazi maalumu isiyochapishwa, Shahada ya Kwanza, Elimu. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kahigi, Kulikoyela. 1977. Sitiari katika Ushairi: Mifano kutoka katika Kichomi. Kazi maalumu isiyochapishwa, Shahada ya Umahiri, Isimu. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kezilahabi, Euphrase. 1974. *Kichomi*. Nairobi: Heinemann.

Lakoff, George. 1993. The Contemporary Theory of Metaphor. Ortony (mh.) 1993, uk. 202-251.

Lakoff, George. 2008. The Neural Theory of Metaphor. Gibbs (mh.) 2008, uk. 17-38.

Leech, Geoffrey N. 1969. *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longmans.

Leech, Geoffrey N. 1981. *Semantics*. tol. 2. Harmondsworth: Pelican Books.

Levin, Samuel R. 1977. *The Semantics of Metaphor*. Baltimore: Johns Hopkins UP.

Nowottny, Winifred. 2000. *The Language Poets Use*. tol. 5. London: Athlone Press.

Nyerere, Julius K. 1968. *Freedom and Socialism / Uhuru na Ujamaa*. Dar es Salaam: Oxford UP.

Ortony, Andrew (mh.). 1993. *Metaphor and Thought*. tol. 2. New York & London: Cambridge UP.

Perrine, Laurence. 1971. Four Forms of Metaphor. *College English* 33/2: 125-138.

Perrine, Laurence. 1977. *Sound and Sense*. 5th ed. New York: Harcourt Brace Jovanovich.

Preminger, Alex & Terry V. F. Brogan (wah.). 1993. *The New Princeton Encyclopedia of Poetry and Poetics*. Princeton: Princeton UP.

Richards, Ivor Armstrong. 1936. *The Philosophy of Rhetoric*. Oxford: Oxford UP.

Ricœur, Paul. 1979a. *The Rule of Metaphor*. London: Routledge & Kegan Paul.

Ricœur, Paul. 1979b. The Metaphorical Process as Cognition, Imagination, and Feeling. Sacks (mh.), uk. 141-57.

Sacks, Sheldon. (mh.). 1979. *On Metaphor*. Chicago: University of Chicago Press.

Semino, Elena & Gerard Steen. 2008. Metaphor in Literature. Gibbs (mh.). uk. 232-246.

Shibles, Warren A. 1971. *Metaphor: An Annotated Bibliography and History*. Whitewater: Language Press.

Ullmann, Stephen. 1962. *Semantics: An Introduction to the Science of Meaning*. Oxford: Blackwell.

Ullmann, Stephen. 1964. *Language and Style*. Oxford: Blackwell.